**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

*Dar es Salaam*
*30 Julai, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

# TAARIFA KWA UMMA

## RAIS SAMIA KUFANYA ZIARA YA KIKAZI NCHINI ANGOLA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ataondoka nchini tarehe 31 Julai, 2026 kwenda nchini Angola kwa ziara ya kikazi ya siku mbili, kwa mwaliko wa Rais wa Jamhuri ya Angola, Mheshimiwa João Manuel Gonçalves Lourenço.

Akiwa nchini humo, Rais Dkt. Samia atafanya mazungumzo na Rais Lourenço na kushiriki hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na Wake wa Marais wa Afrika kwa lengo la kuchangisha fedha kwa ajili ya shughuli za kijamii na kiuchumi, hususan zinazowezesha wanawake na vijana.

Aidha, tarehe 01 Agosti, 2026, Rais Dkt. Samia na mwenyeji wake, Rais Lourenço, watazindua hospitali ya rufaa ya ***Hospital Geral dos Queimados Presidente Julius Nyerere***, jijini Luanda, iliyopewa jina la Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Ziara hiyo ni mwendelezo wa kuimarisha uhusiano wa kihistoria na wa kirafiki kati ya Tanzania na Angola, uliojengwa tangu enzi za harakati za ukombozi wa Bara la Afrika.

Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu